



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Simu: 2988305/2988324
Nukushi: 2988258
Barua pepe: ded@urambodc.go.tz
Tovuti: www.urambodc.go.tz

Mkurugenzi Mtendaji
30 Barabaraya Stend-Boma,
S.L.P 170,
45582 Urambo-Tabora

Unapo jibu tafadhali taja:
Kumb.Na. UDC/V.3/252/VOL.III/92

30.09.2024

TANGAZO

**TANGAZO KWA UMMA WILAYANI URAMBO KUHUSU KUREJESHWA
HUDUMA YA UTOAJI WA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE,
VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1) ya utoaji na usimamizi wa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu za mwaka 2024.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Urambo anatangaza kurejea kwa mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu waenye ulemavu, ambapo jumla ya **TZS. 605,511,446.68** zimetengwa kutolewa katika robo ya 2 ya mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi kwa njia ya mfumo katika Ofisi za Kijiji/Kata zilizopo katika maeneo yao.

Barua zote zitumwe kuititia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mkurugenzi (W), Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 30 Barabara ya Stendi Boma, S.L.P 170 **45582, URAMBO** Simu :0732-988305, na 988324, Nukushi 0732-988258, Barua pepe:ded@urambodc.go.tz, Tovuti www.Urambodc.go.tz

- Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo;-
 - i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na Halmashauri kwa njia ya mfumo wa kieletroniki.
 - ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali na kisiwe kinadaiwa na Halmashauri.
 - iii. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendele na kikundi cha watu wenyewe ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6 a (1) mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyewe ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake.
- Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali: na
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi wenyewe akili timamu na awenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na awnakikundi wenyewe umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kieletroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Barua zote zitumwe kupitia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mkurugenzi (W), Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 30 Barabara ya Stendi Boma, S.L.P 170 45582, URAMBO Simu :0732-988305, na 938324, Nukushi 0732-988258, Barua pepe:ded@urambodc.go.tz, Tovuti www.Urambodc.go.tz

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatanisho vifuatavyo:-

Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kata kwa kuandika jina lake, saini na kugonga muhuri wa Serikali ya Kijiji/Kata, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo wa kieletroniki na taarifa ya akaunti ya benki yenye jina la kikundi au Jina la mtu mwenye ulemavu mmoja aliyekosa wenzake wa kuungana nao (Bank statement)

NB: Kikundi kitakachojumuisha wanakikundi au mwanakikundi ambaye yupo katika vikundi vinavyodaiwa na Halmashauri mikopo ya nyuma, kitakuwa hakina sifa ya kupata mkopo huu.

Mwisho wa kuwasilisha maombi katika mfumo ni tarehe **08/11/2024**.

Tangazo hili limetolewa na :-



Grace Quintine,

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri,
Halmashauri ya Wilaya,
URAMBO.

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMAshaURI YA WILAYA
S.L.P. 170
URAMBO**

Barua zote zitumwe kuitia anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mkurugenzi (W), Halmashauri ya Wilaya ya Urambo, 30 Barabara ya Stendi Boma, S.L.P 170 45582, URAMBO Simu :0732-988305, na 938324, Nukushi 0732-988258, Barua pepe:ded@urambodc.go.tz, Tovuti www.Urambodc.go.tz